

Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

UUNGU UNADHIHIRISHWA

(Nakala hii ni hadithi ya Yesu kutokana na mambo yaliyonukuliwa katika Mathayo 3:13-17 na Yohana 1:31-34 SUV).

Halaiki ya Wayahudi walikuwa wamesimama wakimtzama Yesu akiingia ndani ya Mto Yordani ili abatizwe. Yeye alikuwa amesafiri toka Galilaya ili kufika mahali hapo ambapo Yohana Mbatizaji alikuwa akihubiri na kubatiza watu. Sasa akiwa na umri wa miaka 30 Yesu alikuwa tayari kuanza huduma yake hadharani ili kutimiza kusudi la kiungu la Yeye kufika ulimwenguni. Lakini alipokuwa akianza kuingia majini Yohana Mbatizani akaanza kulalamika na kusema "Mimi sistahili kukubatiza wewe." Lakini Mungu alikuwa amemchagua Yohana ili kumtabulisha Masiha wake ulimwenguni.

Yohana Mbatizaji akamshika Yesu na kumteremsha kinyuma-nyuma na kumtumbukiza majini. Lakini walipokuwa wakitoka majini na huku maji yakinirika usoni mwa Kristo, mbingu zikafunguka na Roho wa Mungu akashuka kama njiwa na kusimama juu yake. Nayo sauti ya Baba Mungu ikanena kutoka Mbinguni huku kila mtu akisikia ikisema: "Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye." Umati wa watu wakapigwa na butwaa na mshtuko mkuu kwa ajili ya Mungu kujidhihirisha kwa njia hiyo ya ajabu. Hapo hapo Yohana Mbatizaji akanena kwa matamshi ya ukweli kabisa na kusema, "Huyu ni Mwana wa Mungu."

Siku hiyo Mungu mkamilifu alikuwa hapo katika Mto Yordani. Mungu Utatu akiwa nafsi tatu aliwakilishwa pale kikamilifu. Nafsi ya Mungu Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, akabatizwa. Naye nafsi ya Mungu aliye Roho Makatifu akashuka kama njiwa. Nayo nafsi ya

Mungu Baba ikanena toka mbinguni. Basi Utatu wa Mungu ukawakilishwa kama nafsi tatu tofauti lakini zenyе umoja katika makusudio yao kama Mungu mmoja.

Utatu wa Mungu ni mafundisho ambayo yanaeleza sifa zake Mungu. Ni mafundisho ya ule umoja wa Uungu—yaani Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu—ambao wote watatu wanashiriki katika Utatu huo. Katika karne zilizopita somo hili lilizusha migogoro mingi ya kithiolojia. Hata katika siku zetu kuna vikundi vingine vinavyojiita vyta Wakristo lakini ambavyo vinakana ukweli wa Utatu wa Mungu. Lakini mafundisho ya Utatu wa Mungu yanasisima na ukweli ufuataa:

1. Kuna Mungu mmoja peke yake.
2. Mungu huyu hudumu milele katika hali tatu tofauti.
3. Baba ni Mungu, Mwana ni Mungu, na Roho Mtakatifu ni Mungu.
4. Baba siye Mwana, Mwana siye Baba, na Baba siye Roho Mtakatifu n.k.

Wale viongozi wa kanisa ambao waliishi kabla ya mukutano ule mkuu wa kanisa wa Nicene (kabla ya 325 Baada ya Kristo —BK) walikiri uungu wa Kristo na kutaja "Baba, Mwana na Roho Mtakatifu." Naye mwanathiolojia wa kanisa aliyejulikana kama Tertullian aliandika mwakani 215 BK na akawa ni kama mwanathiolojia wa kwanza kutumia neno "Utatu wa Mungu" kumweleza Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu kama "wamoja katika nia—wala sio wamoja katika nafsi."

(Endelea katika Ukurasa 2)



**Siku hiyo Mungu
mkamilifu alikuwa
hapo katika Mto
Yordani. Mungu
Utatu akiwa nafsi
tatu aliwakilishwa
pale kikamilifu.**

MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4,
Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,
Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,
Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,
Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,
I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10,
Mt. 25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Inaendelea kutoka Ukurasa

1)

Mgogoro kuhusu uungu na kuzaliwa kwake Kristo ulivuma sana katika karne ya tatu. Katika karne ya nne bwana mmoja aliyejulikana kama Arius alipigia debe mafundisho ya uwongo yaliyosema kwamba Baba aliishi kabla ya Mwanawawe. Yeye alisema kwamba kiasili Kristo hakuwa Mungu na pia kwamba Yeye hakuishi mielele. Wafiasi wa Arius waliamini kwamba Kristo alikuwa kiumbe cha hali ya juu sana ambacho kilumbwa. Mafundisho hayo yakaanza kusambaa kwa haraka.

Wakati Konstantini alipotawazwa kuwa mfalme alifanya Ukristo kuwa dini ya Kirumi na kuita Mkutano wa Kwanza wa Nicaea hapo mwaka 325 AD ili kusuluuhisha mgogoro kuhusu sifa halisi ya Kristo, na ili kueleza uhusiano kati ya Mwana na Baba. Naye bwana mmoja

aliyejulikana kama Athanasius wa huko

Iskanderia ndiye alikuwa kiongozi

wa wale waliosema kwamba Kristo

ni Mungu na kwamba hadhi yake

ilikuwa sawa na ile ya Baba. Hata

ingawa kanisa la wakati huo

lilikuwa limeanguka sana kwa

maswala ya imani idadi kubwa

ya askofu waliokuwa kwenye

mkutano huo (250 katи ya maaskofu

318) walismama wima dhidi ya

mafundisho ya uwongo ya Arius na

kukubaliana na ukweli wa biblia kwamba

Kristo alikuwa Mungu, kwamba alikuwa wa milele,

na kwamba alikuwa sehemu ya Utatu wa Mungu. Basi mkutano huo wa

Nicaea ukakubaliana kuhusu Tamko la Ukweli wa Kikristo uliotokana na

Nicaea ambao ulisema Kristo ni "Mungu wa Mungu, Mwanga wa Mwanga,

Mungu kweli wa Mungu wa Kweli, ambaye alikuwako na hakuumbwu, utu

wake ukiwa mmoja na wa Baba."



Ni jambo la kimsingi kabisa katika dini ya Kikristo kwamba kuna Mungu mmoja ambaye adumu katika utatu. Ikiwa tutakana uungu wa Kristo basi hakutakuwa na msamaha kutokana na dhambi zetu kwa maana damu yake haitakuwa na nguvu kuliko ya mafahali na mbuzi. Lakini sisi tunamshukuru Baba ambaye alimtuma Mwanawawe Yesu duniani ili kufa kwa ajili ya dhambi zetu na ili tuweze kuokoka na kufanyika hekalu ambalo Roho Mtakatifu anaweza kudumu ndani yake. ■

JE, WAPENDEZWA NA KILE AMBACHO UNASOMA?

Kuna nakala za miaka 5 za Ukweli wa Injili
ambazo zimehifadhiwa katika tovuti ya

www.thegospeltruth.org

na zinazoshughulikia zaidi ya mafundisho 20 ya Ukristo.

Gazeti la Ukweli wa Injili ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwashimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tarayi ili uweze kupata toleo la kila kipindii. Gazeti hili la Ukweli wa Injili linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kuitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@thegospeltruth.org

Tahariri



Kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu. Kama vile mmoja wenu, mtunga mashairi alivyosema, Maana sisi sote tu wazao wake. Basi, kwa kuwa sisi tu wazao wa Mungu, haitupasi kudhani ya kuwa Uungu ni mfano wa dhahabu au fedha au jiwe, vitu vilivyo chongwa kwa ustadi na akili za wanadamu. —Matendo 17:28-29

Ni kutokana na Mungu ndipo sisi tuna pumzi na nguvu kwa maana Yeye ndiye Chemichemi ya Uhai. Ni kutokana na Mungu ndipo sisi tuna amani, wokovu, na tumaini la uzima wa milele. Kama wazawa wa Mungu, viumbwe vyenye uhai na akili, hatustahili kusema kwamba Uungu ni kitu kisicho na uhai na ambacho kiliundwa na wanadamu, bali tunahitaji kutambua kwamba Utatu wa Mungu ni kitu chenye urembo mkuu kuliko vitu vingine vyote vilivyo umbwa na ni wenye kustahili ibada zetu.

Katika robo hii ya mwaka ninashughulikia somo la Uungu na tutachunguza maandiko ambayo yanadhihirisha fundisho la Utatu wa Mungu. Mimi najihisi kubarikiwa sana kwa maana sifa za Mungu zimedhihirishwa wazi kuititia kwa yanayosemwa katika Neno la Mungu. Hata ingawa Utatu wa Mungu silo jambo lahisilahuelewa na pia ingawa mifano mingi inayotolewa kueleza Utatu huo haitoshi, ukweli wake ni jambo muhimu sana ikiwa mtu atawenza kuelewa mpango wake Mungu na sababu ya Mungu kuumba wanadamu. Kama ambavyo mwandishi mmoja alisema: "Wewe ukijaribu kueleza Utatu wa Mungu utakuwa kichaa; lakini ukikana ukweli huo utapoteza nafsi yako."

Hebu tafakari kuhusu maandishi ya F.G. Smith kuhusu somo hili kutoka kwa kitabu chake kinacho julikana kama: *Kile Ambacho Biblia Inafundisha* (What the Bible Teaches):

Kwa watu wengi mafundisho ya Utatu wa Mungu huonekana kama kitu ambacho si muhimu, lakini ukweli si huo. Ikiwa Kristo hakuwa Mungu wa kweli na badala yake eti alikuwa mtu mkamilifu basi badala ya Yeye kumleta mwanadamu kwa Mungu kile ambacho alifafulu kuntuonyesha ni jinsi kuliko na pengo kubwa kati yetu na Mungu yule Mmoja. Lakini ikiwa Yeye kwa kweli alikuwa "Mungu aliyedhihirishwa mwilini" kwa ajili ya kumbadilisha mwanadamu mwenye dhambi ili awe na mfano wake, Yeye basi anatuhakikishia ushirikiano na kwamba tunaweza kufanana kitabia na kiroho na yule Baba ambaye anayeishi mbinguni.

Kwa sababu hali ya kweli ya Uungu ni kitu ambacho akili za mwanadamu haiwezi kuelewa msingi wa thiolojia yetu kuhusu Mungu unahitaji kutokana na mambo yale ambayo yamefunuliwa katika Maandiko Mtakatifu. Na kusema kweli tukichunguza Maandiko hatuwezi kamwe kuepuka mafundisho ya Biblia kuhusu Utatu wa Mungu. Tukikosa kuona hayo tutakuwa tumekosea kwa njia kubwa maandiko ambayo yako wazi kabisa yanayohusiana na somo hili (ukurasa wa 45).

Ombi langu ni kwamba msomi wa gazeti hili atakubaliana na urahisi wa Neno la Mungu ambalo linaelezea sifa zake Mungu. Ni baraka kubwa mtu kuwa na ujuzi wa Mungu mmoja ambaye ni utatu na ambaye anafanya na kutenda kazi yake katika maisha yetu ya kila siku.

Mhariri, Michael Smith

Oktoba 2017



Tutembelee

www.thegospeltruth.org

ili kujianidikisha na

kupata jarida

za mbele.

"KWA HIYO, WEWE NDIWE MKUU, EE BWANA MUNGU, KWA MAANA HAKUNA KAMA WEWE, WALA HAPANA MUNGU MWINGINE ILA WEWE, KWA KADIRI TULIVYOSIKIA KWA MASIKIO YETU."

—2 SAMUEL 7:22



Mwongozo wa Kujifunza Biblia

Somo: Utatu wa Mungu

Somo la Biblia: *Kisha wako watatu washuhudiao duniani, Roho, na maji, na damu; na watatu hawa hupatana kwa habari moja.* —1 Yohana 5:7

Muhsasari: Kuna Mungu mmoja pekee. Yeye anaishi milele katika umoja wa watatu—Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Ingawa wote watatu wanaweza kutambuliwa mmoja dhidi ya mwingine kwa nafsi na kwa wajibu wao, wote watatu ni wamoja katika nia na sifa zao.

Maana na maelezo: Utatu wa Mungu ni usemi unaotokana na maneno mawili “Utatu” na “Mungu” na ni maneno yanayolezea hali ya kuwa watatu lakini ambao ni wamoja. Haya ni maneno ya kithiolojia ambayo hutumika kueleza mafundisho ya Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu ambao ni watatu wanaoishi pamoja, wa milele, lakini ambao kwa kweli ni Mungu mmoja.

I. Mungu Mmoja

- A. Kumbukumbu la Torati 6:4 Bwana Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja. (Marko 12:29)
- B. 1 Wakorintho 8:4-6 Mungu ni mmoja tu.
- C. Galatians 3:20 Mungu ni mmoja.
- D. 1 Timotheo 2:5 Mungu ni mmoja.

II. Mungu Baba

- A. 2 Peter 1:17 Maana alipata kwa Mungu Baba.
- B. Waefeso 5:20 Kumshukuru Mungu Baba.
- C. Yohana 6:27 Kwa sababu huyo ndiye aliyetiwa muhuri na Baba, yaani, Mungu.
- D. Warumi 1:7 Neema na iwe kwenu na amani itokayo kwa Mungu Baba yetu.
- E. 1 Petro 1:2 Kama vile Mungu Baba alivyotangulia kuwajua.

III. Mungu Mwana

- A. Yohana 20:28 Bwana wangu na Mungu wangu.
- B. Waefeso 1:8 Lakini kwa habari za Mwana asema, kitii chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele.
- C. Yohana 1:1, 14 Neno (Yesu) alikuwa Mungu.
- D. 1 Timotheo 3:16 Mungu alidhihirishwa katika mwili.
- E. Wafilipi 2:5-6 Yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu.
- F. Mathayo 1:23 Yesu, ambaye ni mwana anaitwa Imanueli yaani, “Mungu pamoja nasi.”
- G. Isaya 9:6 Mwana anaitwa “Mungu mwenye nguvu.”
- H. Wakolosai 2:9 Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili.
- I. Wakolosai 1:15-16 Kristo ni mfano wa Mungu. Yeye ndiye aliumba vitu vyote.

IV. Mungu Roho Mtakatifu

- A. Mwanzo 1:1-2 Roho Mtakatifu alikuwa muumbaji.
- B. Matendo 5:3-4 Kumdanganya Roho Mtakatifu ni kumdanganya Mungu.
- C. 1 Wakorintho 3:16 Roho wa Mungu hudumu katika hekalu la Mungu.

- D. Warumi 8:14 Wale wanaongozwa na Roho ndio wana wa Mungu.

V. Utatu wa Mungu Unadhihirishwa

- A. Mathayo 3:16-17 Baba, Mwana, na Roho Mtakati walikuweko kwa njia dhahiri wakati Yesu alipobatizwa.
- B. Mathayo 28:19 Kubatiza katika jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.
- C. Luka 1:30-35 Utatu wa Mungu waonekana wakati Yesu alipozaliwa.
- D. Matendo 7:54-56 Stefano, akiwa amejaa Roho Mtakatifu, alimwona Yesu amesimama kando kando ya Mungu.
- E. Yohana 14:26 Mungu utatu anadhihirishwa (Yohana 15:26).
- F. 1 Wakorintho 12:4-6 Roho yule mmoja, Bwana, na Mungu.
- G. 2 Wakorintho 13:14 Sehemu tofauti za Mungu zinatajwa kwa njia iliyo wazi.
- H. Waefeso 4:4-6 Roho Mmoja, Bwana, na Baba.

VI. Umoja wa Utatu wa Mungu


- A. Mwanzo 1:26-27 Mwanadamu aliumbwa kwa mfano na maumbile ya utatu wa Mungu (Mwanzo 3:22).
- B. 1 Yohana 5:7 Baba, Neno (Yesu), na Roho Mtakatifu ni wamoja.
- C. Yohana 10:30; 17:11, 22 Yesu na Baba ni wamoja.
- D. Yohana 10:38 Baba yu ndani ya Yesu naye Yesu yumo ndani ya Baba.
- E. Yohana 12:44 Kumwamimi Yesu ni kumwamini Baba.
- F. Yohana 14:8-11 Kumwona Kristo ni kumwona Baba.

Tamati

Yesu akamjibu, ya kwanza ndiyo hii, sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja. —Marko 12:29

UUNGU WENYE UTATU

Biblia inafundisha wazi kwamba kuna Mungu mmoja wa kweli ambaye yuko hai na ambaye ndiye muumbaji wa ulimwengu—Mungu wa milele, amri jeshi mkuu, asiyebadilika, mwenye nguvu zote, mwenye hekima, haki, na mtakatifu. Lakini pia Biblia inafundisha kwamba Baba ni Mungu, Yesu ni Mungu, na Roho Mtakatifu ni Mungu. Kwa lugha ya kithiolojia uhusiano huu wa Mungu mmoja, lakini ambaye ni mwenye nafsi tatu za kiungu, unajulikana kama Utatu wa Mungu.



Hata ingawa neno Utatu wa Mungu halipatikani katika Maandiko dhana ambayo maneno hayo yanawakilisha inapatikana kote katika Biblia. Yule MUNGU MMOJA huonekana kwa njia ya watatu ambao wanaishi pamoja, wa milele, wenyе hadhi moja, na wenyе nguvu sawia. Zaidi ya hayo (wao) wako wamoja kwa roho, kwa nia, kwa kudumu, na kwa sifa zao – hata ingawa pia wao ni watatu katika nafsi, kimawazo, na kiwajibu.

Kanuni na wazo la Utatu ni wazo lililojaa fumbo na ni jambo ambalo linaweza kuwa ngumu mtu kuelewa kikamilifu. Lakini Mungu ni mkuu zaidi kuliko wanadamu. Akili zake mwanadamu zikiwa peke yake haziwezi kuelewa kina na ukamilifu wake Mungu. Pia ni jambo muhimu mtu kuelewa kile ambacho Biblia inasema

kuhusu swala hili kwa maana wokovu na uhifadhi wa nafsi ya mwanadamu hutegemea ukweli na uhalali wa utatu wake Yeye ambaye ni mwenye Uungu.

Mungu ni Mungu Mmoja

Wakati Yesu aliuilizwa kuhusu amri ya kwanza jibu lake lilikuwa, "Yesu akamjibu, ya kwanza ndiyo hii, sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja" (Marko 12:29). Hii ni kusema kwamba, "Yehova, Mungu wetu, ni Yehova mmoja." Mataifa mengine waliabudu miungu mingi lakini Mungu wa Wayahudi aliquwa mmoja. Huku akinakili Kumbukumbu la Torati 6:4 Yesu alikariri ukweli kwamba kuna Mungu mmoja tu aliye wa kweli. Mungu yule wa Agano la Kale ndiye pia Mungu wa Agano Jipy. Imani inayohusu Mungu mmoja ni ukweli wa kimsingi wa Neno la Mungu na thiolojia yetu kuhusu Mungu haistahili kamwe kuwa na imani kwamba kuna miungu mitatu tofauti. Mtume Paulo naye akasema katika 1 Wakorintho 8:4, "Hakuna Mungu ila mmoja tu." Ukweli huo unasemwa tena katika Wagalatia 3:20, "Mungu ni mmoja" na katika 1 Timotheo 2:5 ambayo pia inasema, "Mungu ni mmoja."

Mungu ni Utatu

Mungu (ambaye ni mmoja) ni Mungu utatu. Uungu wake Mungu humjumuisha Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, "Kwa maana wako watatu washuhudiao mbinguni, Baba, na Neno, na Roho

(Endelea katika Ukurasa 6)



**“Baba, Mwana, na
Roho Mtakatifu ni
nafsi tatu ambazo
hudumu katika
umoja kamili kama
Mungu. Majina hayo
sio majina tofauti ya
sehemu tofauti za
Mungu, kwa maana
wao ni Mungu, na
Mungu ni mmoja.”**

(Inaendelea kutoka Ukurasa 5)

Mtakatifu, na watatu hawa ni umoja” (1 Yohana 5:8). Andiko hili linatangaza (kwa njia wazi kabisa) kuhusu wingi wa Mungu, na umoja ulioko katika sifa halisi ya kiungu ya Mungu. Kila mshiriki wa Uungu anatajwa kama nafsi tofauti katika Biblia—Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu.

Mungu Baba

Mungu Baba ametajwa katika maandiko mengi katika Biblia. Yesu alisema kumhusu “Baba, yaani, Mungu” katika Yohana 6:27. Mtume Paulo akawaandikia kusanyiko la Rumi na kusema: “Neema na iwe kwenu na amani itokayo kwa Mungu Baba yetu” (Warumi 1:7). Naye Petro akasema kuhusiana na Yesu kwamba “alipata kwa Mungu Baba heshima na utukufu” (2 Petro 1:17). Petro pia akasema kuhusu (jinsi) “Mungu Baba aliviyotangulia kuwajua” (1 Petro 1:2). Basi ni dhahiri kwamba Baba Mungu alikuwa nafsi binafsi ambayo Kristo na mitume walinena kuhusu.

Mungu Mwana

Yesu Kristo pia alitajwa sana katika Agano la Kale na Agano Jipywa kuwa ni Mungu. Hata ingawa watu wengi hukana uungu wake Kristo au kufundisha kwamba Yeye alikuwa Baba, Neno lake Mungu linafundisha kwamba Yesu alikuwa sehemu binafsi ya Uungu. Nabii Isaya aliandika na kusema: “Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, . . . Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu” (Isaya 9:6). Naye malaika wa Bwana akamtokea Yusufu na kusema kwamba Maria atamzaa mtoto wa kiume, “Nao watamwita jina lake Imanueli; yaani, Mungu pamoja nasi” (Mathayo 1:23). Na kwa maneno ya kuvutia Yohana 1:1, 14 inasema kwamba, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno (Yesu), naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu . . . Naye Neno (Yesu) alifanyika mwili, akaka kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa

Baba; amejaa neema na kweli.” Yeye alikuwako tangu mwanzo, “Lakini kwa habari za Mwana asema, kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele” (Waebrania 1:8). Yesu, ambaye alitumwa kutoka kwa Baba, alikuwa Mungu, na akafanyika mwili kati yetu (Warumi 9:5). “Na bila shaka siri ya utauwa ni kuu. Mungu alidhihirishwa katika mwili” (1 Timotheo 3:16). Tomaso alipomwona Yesu (baada ya kusulubiwa kwake) alimwita “Bwana wangu na Mungu wangu” (Yohana 20:28). Yesu alikuwa Mungu kwa hali na sifa (Wafilipi 2:5-6) na “katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili” (Wakolosai 2:9). Bila shaka kuna ushahidi mwingi kutoka kwa Biblia ambaeo unadhihirisha kwamba Yesu ni wa milele na kwamba Yeye ni Mungu.

Mungu Roho Mtakatifu

Roho Mtakatifu ndiye sehemu ya tatu ya Utatu wa Mungu. Hapo mwanzo wakati ulimwengu uliumbwu Roho Mtakatifu alikuwa pale kama muumbaji; “Hapo mwanzo Mungu alizumba mbingu na nchi. . . . Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji” (Mwanzo 1:1-2). Roho Mtakatifu amedhihirishwa kama Mungu katika Matendo 5:3-4, “Petro akasema, Anania, kwa nini Shetani amekujaza moyo wako kumwambia uongo Roho Mtakatifu, . . . hukumwambia uongo mwandanadamu, bali Mungu.” Ushahidi mwingine wa Mungu Roho Mtakatifu unapatikana katika 1 Wakorintho 3:16, “Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?” Je, ni nani anaishi katika hekalu au katika makazi yake Mungu isipokuwa Mungu mwenyewe? Ni Mungu Roho Mtakatifu ndiye anadumu katika miili yetu ambayo ni hekalu za kidunia za Mungu. Roho Mtakatifu, akiwa Mungu, anafanya kazi yake kama Mungu, kazi ya kuita watakatifu wa Mungu na kuwapatia vipawa vya kiungu (Matendo 13:2). Uungu wake pia unadhihirishwa katika Warumi 8:14: “Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu.”

Watatu Ndani ya Mmoja

Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni nafsi tatu ambazo hudumu katika umoja kamili kama Mungu. Majina hayo sio majina tofauti ya sehemu tofauti za Mungu, kwa maana wao ni Mungu, na Mungu ni mmoja. Ukweli wa wingi wao unaonyeshwa na kudhihirika katika maandiko mengi. Wakati malaika alimtokea Maria (kama ambavyo imenakiliwa katika Luka 1:30-35) ujumbe wake ultaja washirika wote wa Utatu wa Mungu. Mungu Baba alikuwa kama kivuli kwake, naye Roho Mtakatifu akashuka juu yake ili apate mimba ya Mwana wa Mungu. Unabii ukatolewa kwamba Bwana Mungu angempatia Mwanawe kiti cha enzi na kwamba ufalme wa Mwanawe haungefika kikomo.

Walidhihirishwa Wakati Yesu Alibatizwa

Nafsi zote tatu za Uungu wa Mungu zinapatikana kwa hali moja au nyininge katika nakala ya ubatizo wake Yesu katika Mathayo 3:16-17. Roho Mtaktifu alishuka kama njiwa na kutua mwilini mwake Yesu, halafu sauti ya Baba ikanena toka mbinguni. Ni dhahiri kwamba hawa walikuwa nafsi tofauti na jambo hili linaonyesha upotovu uliopo katika mafundisho kwamba Mungu Baba na Yesu ni nafsi moja.

Yesu alifundisha wanafunzi wake kubatiza "kwa jina la Baba, la Mwana, na la Roho Mtakatifu" (Mathayo 28:19). Tamshi hili linajumuisha kila nafsi ya Mungu. Nafsi hizo tatu za Mungu zilidhihirishwa wakati Yesu alisema na wanafunzi wake kuhusu kuja kwake Roho Mtakatifu. "Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia" (Yohana 14:26).

Walidhihirishwa Stefano Alipopigwa Mawe

Uungu ulidhihirishwa wakati Stefano alikuwa akipigwa kwa mawe katika Matendo 7:54-56. Stefano alikuwa amejaa Roho Mtakatifu na kutazama juu akamwona Yesu amesimama katika mkono wa kulia wa Mungu (Baba). Biblia inasema kuhusu vipawa tofauti, kazi tofauti, na huduma tofauti lakini inasema kwamba ni Roho yule yule, Bwana mmoja, na Mungu yule mmoja (1 Wakorintho 12:4-6). Waefeso 4:4-6 inafundisha kwamba kuna Roho mmoja, Bwana mmoja, Mungu Mmoja ambaye ni Baba wa wote. Basi

Mungu utatu, kama nafsi tatu tofauti, ni jambo linalofundishwa vizuri katika maandiko matakatifu.

Umoja wa Utatu wa Mungu

Ingawa Utatu wa Mungu ni wa "watatu" Mungu mwenyewe ni mmoja. Kama mmoja wao angeondolewa basi kusingekuwa na Mungu. Hii ni moja ya fumbo na kizungumkuti cha Mungu, kwa maana wao hawawezi kutenganishwa mmoja kwa mwingine. Umoja wa Utatu wa Mungu pia umeonyeshwa katika maandiko mengi ya Biblia. Katika Mwanzo 1:26 tunasoma, "Mungu akasema, na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu" Hii ilionyesha uwepo wake Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Mwanzo 1:27 inasema, "Mungu akaumba mtu kwa mfano wake." Hapa basi tunaona umoja huo wa Mungu.

Yesu alizungumza kuhusu umoja wake na Baba yake wakati mwingi, "Mimi na Baba tu umoja" (Yohana 10:30). "Baba yu ndani yangu, nami ni ndani ya Baba" (Johana 10:38). Pia aliombea umoja wa wanafunzi wake ili "wawe na umoja kama sisi tulivyo" (Yohana 17:11,22). Katika Yohana 12:44 Yesu alisema, "Yeye aniaminiye mimi, haniamini mimi bali ye ye aliyenipeleka [Baba]." Filipo naye akamwomba Yesu amwonyeshe Baba, naye Yesu akamjibu kwa kusema, "Filipo akamwambia, Bwana, utuonyeshe Baba, yatutosha. Yesu akamwambia, Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Aliyeniona mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba? Husadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu? Hayo maneno niwaambiayo mimi siyasemi kwa shauri langu; lakini Baba akaaye ndani yangu huzifanya kazi zake. Mnisadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu."

Mafundisho ya Neno la Mungu ni Dhahiri

Mafundisho ya Uungu, yaani Utatu wa Mungu, ni mafundisho yaliyofundishwa waziwazi katika Neno lake Mungu, hata ingawa kuna sehemu ambayo ni vigumu mtu kuelewa. Mambo ambayo sio dhahiri katika Maandiko huonekana kwamba hayana umuhimu mwingi, na watu wakijadili kuhusu mambo ambayo hayajafundishwa katika Neno la Mungu

(Endelea katika Ukurasa 8)



"Ingawa Utatu wa Mungu ni wa "watatu" Mungu mwenyewe ni mmoja. Kama mmoja wao angeondolewa basi kusingekuwa na Mungu. Hii ni moja ya fumbo na kizungumkuti cha Mungu, kwa maana wao hawawezi kutenganishwa mmoja kwa mwingine."


(Inaendelea kutoka Ukurasa 7)

litakuwa ni jambo ambalo linaweza kuleta madhara makuu. Lakini ikiwa mtu atakana ukweli wa mafundisho ya Utatu wa Mungu mwishowe atakuwa wa kukana uungu wake Mwana wa Mungu, au atakana nguvu za kiungu na uwezo unaotokana na Roho Mtaktifu. Kuna Mungu mmoja. Kuna washirika watatu wa uungu: Mungu Baba, Mungu Mwana, Mungu Roho Mtaktifu. Kuna Mungu mmoja wa milele ambaye aishi. Wakristo wanastahili kufurahi na kumtukuza Mungu huyo ambaye amefanya (na anaendelea kufanya) mambo makuu kwa niaba ya watoto wake.

“Jinsi zilivyo kuu utajiri na hekima na maarifa ya Mungu! Hukumu zake hazichunguziki, wala njia zake hazitafutikani! . . . Kwa kuwa vitu vyote vyatoka kwake, viko kwa uweza wake, tena vinarejea kwake. Utukufu una ye ye milele. Amina” (Warumi 11:33, 36). Tunakwabudu ewe Mungu—Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. ■

KAZI YA KIBINAFSI YA UTATU WA MUNGU

**“BABAA NDIYE HUPANGA MPANGO,
YESU NAYE HUFANYISHA MPANGO HUO WA BABAA KAZI,
ROHO MTAKATIFU NAYE HUSIMAMIA MPANGO UNAPOTEKELEZWA.”**



Baba, Mwana, na Roho Mtaktifu wana umoja wa kuwa pamoja kama Mungu, na wao hufanya kazi kwa umoja katika ulimwengu huu, na pia katika maisha ya wanadamu. Ingawa washirika wa Uungu wa Mungu wana malengo na makusudi sawa, na pia wana sifa na kazi sawa, kila mshirika wa Utatu wa Mungu huwa na wajibu maalum na kazi maalum. Mwandishi mmoja alitoa muhstasari wa wajibu wa Utatu wa Mungu na kusema yafuatayo: “Baba ndiye hupanga mpango, Yesu naye hufanyisha mpango huo wa Baba kazi, Roho Mtakatifu naye husimamia mpango unapotekelezwa.” Mungu baba ni upendo. Yeye ndiye chimbuko na mpangaji mkuu wa mpango wa wokovu. Baba ndiye alituma mwanawe ili kutimiza mpango

wake wa kuwakomboa wanadamu. Naye Yesu akamtii Baba kwa kuchukua mfano wa mwili na kufa msalabani ili kwa damu yake ulimwengu uweze kuokolewa kutoka dhambini. Yesu basi akawa ni daraja kati ya Baba na wanadamu, na ye ye sasa ni kuhani mkuu na mpatanishi wa watu wa Mungu. Yeye pia ni mwokozi wa ulimwengu na kichwa cha kanisa.

Roho Mtakatifu (ambaye alitumwa kutoka kwa Baba) naye hukakikishia wanadamu kuhusu dhambi, anawafunza, anawaongoza, na pia anawafariji. Yeye hutakasa na kudumu katika miyo ya watu wa Mungu. Roho ndiye huwapatia watu nguvu na kuwawezesha kuishi kulingana na mapenzi yake Baba.

“Neema ya Bwana Yesu Kristo, na pendo la Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu ukae nanyi nyote.”

—2 Wakorintho 13:14



SIFA ZAKE MUNGU

Sura ya kwanza ya Biblia imeanzia na maneno yafuatayo: "Hapo mwanzo Mungu . . ." Neno la Mungu limeweka wazi kwa wanadamu wote tabia za Mungu na sifa ambazo Yeye mwenyewe alichagua kutufahamisha. Mipango ya Mungu na mapenzi yake na hata hukumu zake huleta ufahamu, na pia kumletea wanadamu mwelekeo. Maisha ya wanadamu huwa maradifu na yanapata maana wakati wanadamu huyo amejifunza na kuelewa vizuri sifa za Mungu.

MUNGU...

Hana mwili

Kimaumbile Mungu hana mwili

"Mungu ni Roho." —Yohana 4:24

Ana uhai ulio ndani yake

Yeye hakuumbwa na hana mwisho.

Yeye ndiye wa kweli na halisi.

"Mungu akamwambia Musa, MIMI NIKO AMBAYE NIKO" —Kutoka 3:14

Amejitosheleza

Mungu hana haja ya kitu
kingine kando yake.

"Baba . . . ana uzima nafsini
mwake." —Yohana 5:26

Ni wa milele

Mungu hana mwanzo na
hatakuwa na mwisho. Yeye hana
tamati na atadumu milele.

"Kabla haijazaliwa milima, wala
hujiumba dunia, na tangu milele hata
milele ndiwe Mungu." —Zaburi 90:2

Hana mwisho

Hawesi kupimika, hana
mipaka, hana vizuizi

"Bwana wetu ni mkuu na mwingi wa nguvu,
akili zake hazina mpaka." —Zaburi 147:5

Ni Mungu Utatu

Mungu hujidhihirisha kwa wanadamu
kama Mungu nafsi tatu—Baba,
Mwana, Roho Mtakatifu.

"Kwa maana wako watatu washuhudiao
mbinguni, Baba, na Neno, na Roho Mtakatifu,
na watatu hawa ni umoja." —1 Yohana 5:7

Ni mmoja

Mungu ni mmoja na hawesi kugawanywa.
Kuna Mungu mmoja wa kweli anayeishi.

"Bwana Mungu wetu ni Bwana
mmoja." —Marko 12:29

Ni mfalme

Mungu ndiye mwenye mamlaka yote na
nguvu zote na ndiye anayetawala wote.

"Kwa kuwa Bwana ni Mungu mkuu, na Mfalme
mkuu juu ya miungu yote." —Zaburi 95:3.

Mwenye vivu

Mungu hupendezwa na ibada na sifa
ambazo Yeye anastahili kwa kweli.

"Maana hutamwabudu mungu
mwingine, kwa kuwa Bwana, ambaye
jina lake ni mwenye vivu, ni Mungu
mwenye vivu." —Kutoka 34:14.

Hababili

Mungu hababili na anaweza
kutegemewa na kuaminika.

"Kwa kuwa mimi, Bwana, sina
kigeugeu." —Malaki 3:6



(Inaendelea kutoka Ukurasa 9)

Yuko kila mahali

Kila wakati Mungu yuko karibu
nasi na pia yuko kila mahali.

“Je, mtu ye yote aweza kujificha mahali
pa siri, nisimwone? Asema Bwana. Je!
Mbingu na nchi hazikujawa nami?
Asema Bwana.” —Yeremia 23:24

Ni mwenye nguvu zote

Mungu ni mwenye nguvu
zote na mamlaka yote.

“Nimepewa mamlaka yote mbinguni
na duniani.” —Mathayo 28:18

Ajua mambo yote

Mungu anajua mambo yote na ufahamu
wake ni mkamilifu. Yeye anajua
yaliyopita, yaliyoko, na yatakayokuja.

“Wala hakuna kiumbe kisichokuwa wazi
mbele zake, lakini vitu vyote vi utupu
na kufunuliwa machoni pake yeye aliye
na mambo yetu.” —Waebrania 4:13

Ni mwenye hekima

Mungu anajua mambo yote kwa
undani sana na kuyaelewa, anajua
kinachofaa katika kila hali.

“Danieli akajibu, akasema, na lihimidiwe
jina la Mungu milele na milele; kwa kuwa
hekima na uweza ni wake.” —Danieli 2:20

Ni mwenye upendo

Mungu hushughulishwa sana na hali
ya mwanadamu. Upendo ndio sifa kuu
ya wasifa wake Mungu. Upendo huu
sio wa kihisia tu bali ni kwa matendo.

“Nasi tumelifahamu pendo alilo nalo
Mungu kwetu sisi, na kuliamini. Mungu
ni upendo, naye akaaye katika pendo,
hukaa ndani ya Mungu, na Mungu
hukaa ndani yake.” —1 Yohana 4:16

Ni mtakatifu

Mungu ni mtakatifu na ni
mkamilifu kwa tabia na usafi. Yeye
ametenganishwa kabisa na dhambi
zote, uovu wote, na uchafu wote.

“Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi
ni mtakatifu.” —1 Petro 1:16

Ni wa haki

Mungu hushughulikia kila kitu kwa haki
kulingana na kile kinachofaa na kizuri

“Haki na hukumu ndio msingi wa
kiti chako.” —Zaburi 89:14

Ni mwema

Mungu ni mwenye fadhili, mtenda
wema na mwenye kujaa baraka.

“Wema wa Mungu wakuvuta upate
kutubu.” —Warumi 2:4

Ni mwaminifu

Mungu habadiliki, ni wa kutegemewa,
mkweli, hawezি kusema uongo.

“Basi jueni ya kuwa Bwana, Mungu wenu,
ndiye Mungu; Mungu mwaminifu.” —
Kumbukumbu la Torati 7:9

Ni mwenye rehema

Mungu ni mwenye msamaha,
huruma, na huwajali watu.

“Bwana amejaa huruma na neema, haoni hasira
upesi, ni mwingi wa fadhili.” —Zaburi 103:8

Mwenye neema

Mungu ni mkarimu na mwenye
kutoa vipawa ambavyo wale
wanaopewa hawavistahili.

“Maana neema ya Mungu iwaokoayo
wanadamu wote imefunuliwa.” —Tito 2:11

Hana mfano

Mungu hafananishwi na chochote.
Hakuna mwenye kimo chake
na ni Mungu mkamilifu.

“Mtanifananisha na nani, basi, nipate
kuwa sawa naye? Asema yeye aliye
Mtakatifu” —Isaya 40:25

Maswali na Majibu

Kusema kwamba Kristo alikuwa muungano kamili wa mwanadamu na Mungu ni kumaanisha nini?

Yesu Kristo alikuwa mtu mmoja ambaye ndani yake mlikuwa na asili mbili—ya kiungu na ya kibinadamu. Usemi huu unaeleza umoja wa uwanadamu wa Kristo na uungu wake katika mtu mmoja au katika maisha ya nafsi moja. Yesu ni Mungu katika mwili: “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu . . . Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; ameja neema na kweli.” (Yohana 1:1, 14). Yesu alikuwa na asili mbili—asili ya Mungu na ya mwanadamu. Yeye hakuwa nusu Mungu na nusu mwanadamu bali alikuwa Mungu kamili na mwanadamu kamili. Na alipofanyika mwanadamu Yesu hakupoteza uungu wake bali aliendelea kudumu duniani kama Mungu ambaye pia alikuwa na asili ya mwanadamu.

Je, Utatu wa Mungu unaweza kufafanuliwa kwa njia gani?

Kuna mifano mingi ambayo imetumiwa kufafanua wazo la Utatu wa Mungu. Lakini nyingi ya mifano hiyo haina uwezo wa kumdhihirisha Mungu akiwa nafsi tatu ndani ya Mungu mmoja na tunahitaji kuchukua mifano hiyo kama mifano isiyofaa kwa maana matumizi ya minge ya mifano kama hiyo huletea watu maoni yasiyofaa kuhusu Utatu wa Mungu.

Wakati mwingi yai hutumiwa kama mfano wa kufafanua Utatu wake Mungu. Yai la kuku lina sehemu tatu: sehemu ya nje ambayo ni ngozi, sehemu nyeupe ya ndani, na sehemu ya manjano iliyo ya ndani kabisa. Sehemu hizo zote ndizo huitwa yai. Umoja wa sehemu hizo huwa kitu kimoja. Lakini ikilinganishwa na Utatu wa Mungu yai haliwezi kusimamia Utatu wa Mungu kwa sababu sehemu ya manjano ya yai ikiwa peke yake sio yai kamili, kama vile ambavyo kila mmoja wa Utatu wa Mungu ni Mungu kamili. Kristo ni Mungu mkamilifu, lakini pia Mungu ni Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Kimaumbile, wao ni wamoja kinyume na sehemu tofauti za yai. Vile vile tunda la tofa lina sehemu ya ngozi, ya mwili, na pia mbengu zake. Lakini hata mfano huo haufai (kama ambavyo mfano wa yai haufai) kwa maana kila mmoja wa Utatu wa Mungu kivyake ni Mungu.

Mfano mwininge ambao hutumika ni maji. Maji yanaweza kuwa kama barafu, kama maji, na kama gesi. Kimaumbile na kiumuundo hali hizo zote huwa zinafanana kabisa. Lakini maji yakiwa kama maji hubaki katika hali hiyo ya umaji-maji, yakiwa barafu yanabaki kuwa barafu, na yakiwa gesi yanabaki kuwa gesi—ilhali Utatu wa Mungu katika ukamilifu wake unakuwepo kila wakati. Hata ingawa barafu inaweza kubadilika na kuwa majimaji, kamwe Mwana hawezu kuwa Baba n.k.

Mfano mwininge ambao hutumika ni ule wa mwanaume akiwa kwenye wajibu wake wa baba, mwana, na mume kwa wakati mmoja. Lakini mfano huu unaonyesha utatu wa majukumu ya mwanaume na hautoshi kudhihirisha jinsi nafsi tatu za Utatu wa Mungu zilivyo tofauti.

Ni kwa nini Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu wanaitwa nafsi?

Mungu ni utatu wa nafsi tatu: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Wao sio nafsi moja lakini wakiwa pamoja wanakuwa Mungu mmoja. Baba sio Mwana, Mwana sio Roho, lakini kila mmoja wao ni Mungu. Jambo hili limefafanuliwa katika ‘ngao’ ya Utatu wa Mungu ambayo inapatikana katika ukurasa wa 5.

Hawa sio ‘wanadamu’ wa kawaida ambao wako na miili ya kibinagsi, lakini muktadha wa msemo huu ni kuwamba wao wanajijua kibinagsi, wanaweza kusema, wanaweza kupenda, wanaweza kuwa na nia ya kufanya jambo fulani nk. Hizi ndizo sifa za mtu na nafsi yake, ndiposa neno nafsi linatumika kusema kuhusu Utatu wa Mungu.

Dkt. Henry Morris anasema kwamba kimaumbile ulimwengu huwa katika hali ya utatu. Ndani mwake kuna vitu tatu: vitu ambavyo huwa na mwili, sehemu ambayo iko wazi, pia ulimwengu una muda au wakati. Ukitoa moja ya mambo hayo matatu ulimwengu utakoma kuendelea. Lakini hata ingawa mfano huu unaonyesha vile ambavyo vitu hivyo vitatu vina uhusiano kila kimoja kwa vingine vitu hivyo haviko kamili kipekee kama vile ambavyo kila mmoja wa washirika wa Uungu wa Mungu alivyo kamili.

Michoro ya kijometri pia hutumiwa kufafanua Utatu wa Mungu. Kwa mfano mchoro wa pembe tatu una sehemu tatu zilizo huru ambazo zimeungana kuunda mchoro mmoja. Lakini mfano huo pia haufai kwa sababu kila mstari ukiwa peke yake sio mchoro wa pembe tatu.

Ingawa sio hatia mtu kujaribu kuelewa Utatu wa Mungu katika akili zake uelewaji wa aina hiyo unaweza kumpotosha mwanadamu. Mfano hiyo yote haitoshi na haidhihirishi uwepo wa Utatu wa Mungu kwa maana Mungu (ambaye hana kipimo) hawezu kuelezwu vizuri kwa kutumia vitu vyenye vipimo. Mafundisho ya Utatu wa Mungu ni ufunuo wa Mungu na sio dhana ambayo inaweza kudhihirisha kwa kutumia maumbile au kwa kutumia akili.



JE, WAJUA?

Baadhi ya madhehebu ya Kikristo hayaungi mkono dhana ya Utatu wa Mungu, na badala yake wanaikataa. Hata ingawa madhehebu hayo sio mengi, makubwa kati ya madhehebu hayo ambayo hayaungi mkono dhana ya Utatu wa Mungu ni Kanisa la Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho (Church of Jesus Christ of Latter-day Saints, yaani Mormons, au Wamomoni) na Mashahidi wa Yehova (Jehovah's Witnesses).

Mashahidi wa Yehova husema kwamba Yesu alikuwa na mwanzo na kwamba Yeye aliumbw na Mungu. Wao pia hawaamini kwamba Roho Mtakatifu ni nafsi, na badala yake wao huamini kwamba Roho Mtakatifu ni nguvu za Mungu. Wamomoni nao hufundisha kwamba Mungu alimuumba Kristo na kwamba Uungu ni kamati ya miungu watatu amba ni tofauti. Kwa kweli mafundisho hayo yao ni dhana ya miungu watatu badala ya mafundisho ya Biblia ambayo ni ya Mungu mmoja pekee.



HEBU NIMWONE YESU PEKE YAKE

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA

Wakainua macho yao, wasione mtu ila Yesu peke yake. —Mathayo 17:8

Pale mlimani wakati Yesu alibadilishwa Yeye alionekana akizungumza na Musa na Eliya—Musa akiwakilisha sheria ilhalii Eliya alikuwa akiwakilisha manabii; huku Yesu akiwakilisha kipindi kipycha neema. Huku akiwa amepigwa na mshangao mkubwa na ari kuu, Petro alijitolea kuunda hema tatu, moja kwa kila mmoja wa watu hawa. Lakini wingu jeupe likawatia uvuli na Baba akanena: "Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye" (mstari wa 5). Na huku wakiwa na woga mkuu wanafunzi walianguka kifulifuli na wakati walipoinua nyuso zao hawakumwona mtu mwengine isipokuwa Yesu.

Kuna vikundi vingi, vuguvugu, huduma tofauti, na hata watu binafsi amba hukazana ili sisi tuwe makini kwao na tuwe waaminifu kwao. Hata ingawa kuna idara ambazo zinafaa, na hata watu amba tunastahili kuwa makini kwao, Kristo peke yake pamoja na Baba ndio wanastahili kupewa ibada zetu na kujitolea kwetu. Haistahili iwe kwamba sheria au manabii ndizo zinatusukuma kufanya huduma, bali ni Kristo peke yake. Hata tukiwa katika vipindi shwari maishani au vipindi vyenye ugumu tunahitaji kuwa na maono mapya ya kutuwezesha kutomwona mtu mwengine isipokwa Kristo peke yake. Na katika ulimwengu amba una sauti nyingi tunahitaji kuisikia sauti ya Mwana wa Mungu peke yake.



Mradi tunakazia macho yetu kwa wanadamu au kwa hali zinazotuzunguka tutafanyika kuwa watu waliokata tamaa na wenye kufa moyo. Enyi wenzangu mlio askari wa msalaba wa Yesu kazeni macho yenu kwa Yesu. Hebu Yeye awe ndiye msukumo wa kazi zetu na sadaka zetu, kwa maana Yeye ndiye atawea kutuvusha maishani haya kwa ushindi wake. Kama ambavyo wimbo unavyosema: "Hebu nimwone Yesu peke yake." ■